


JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

TUME YA TAIFA YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Telegramu: COSTECH
Simu: +255 (022) 2771358
Mkurugenzi Mkuu: +255 (022) 2774023
Idara ya Utafiti: +255 (022) 2700749
Barua pepe: dq@costech.or.tz



Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S. L. P. 4302
Dar es Salaam
Tanzania

TAARIFA KWA UMMA

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) inapenda kuujulisha Umma wa Watanzania kuwa katika kuendeleza utamaduni wa kuadhimisha Siku ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu imeandaa Majadiliano maalum wa Kisayansi Siku Jumatatu ya tarehe 06 Julai, 2020, yenye kaulimbiu ya ***“Utafiti na Ubunifu ni Msingi wa Kukuza Uchumi wa Viwanda kwa Ajira na Biashara Endelevu.”***

Aidha Tume kwa kutambua umuhimu Sayansi, Teknolojia na Ubunifu katika kuendeleza ukuaji wa Sekta ya Viwanda nchini inashiriki Maonyesho ya 44 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam, itawakutanisha wadau wake wakiwemo watafiti, wabunifu, wajasiriamali, sekta binafsi, na umma kwa ujumla ili kujadili masuala mtambuka yanayosaidia kuendeleza sekta hii muhimu.

Katika majadiliano haya, mada kuu tatu zitajadiliwa ambazo ni:

- (i) Kubadilishana uzoefu unaotokana na ushiriki katika ubunifu na ujasiriamali,
- (ii) Mchango wa Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STU) katika kuchochea maendeleo ya sekta ya viwanda na
- (iii) Nini kifanyike kuwezesha sekta binafsi kuongeza ushiriki katika kuchangia maendeleo ya utafiti na ubunifu.

Majadiliano haya yatafanyika katika Viwanja vya Mwl. J.K. Nyerere- Sabasaba, Dar es Salaam, katika Ukumbi wa **Kawawa (DOME) kuanzia Saa 3:00 kamili asubuhi mpaka saa 9:00 kamili Alasiri.**

Nyote mnakaribishwa.

Imetolewa na:

**Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu
COSTECH**